**KINNAPA DEVELOPMENT PROGRAMME BIO.**
**P.O BOX 83 PARTIMBO,KIBAYA,KITETO-MANYARA**
**Email** : info@kinnapa.or.tz : **Website** : www.kinnapa.or.tz

**KINNAPA Development Programme** ni Shirika lisilo la Kiserikali linaloundwa na wananachama 5,800 kutoka kwenye jamii za wafugaji, wakulima wadogo wadogo na wawindaji waokota matunda.

Jina **KINNAPA** ni ufupisho wa vijiji sita vilivyoanzisha shirika hili yaani Kibaya, Kimana, Njoro, Ndaleta, Namelock and Partimbo. Na kwa lugha ya Kimaasai KINNAPA inamaanisha '**kubebana**' au '**kusaidiana**'.

Shirika hili lilianzishwa mwaka 1990 na wanajamii kutoka katika vijiji sita vilivyotajwa hapo juu ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya ardhi hasa kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. **KINNAPA ilisajiliwa** rasmi tarehe **30/01/1992**. Hivyo Shirika hili lina zaidi ya miaka **31** sasa.

Mafanikio ya Shirika hili yametokana na umoja wa wana jamii katika kulinda ardhi yao, kutambua haki zao na umuhimu wa maendeleo katika kuboresha maisha yao na ya vizazi vinavyokuja.

Mkutano Mkuu wa Shirika la **KINNAPA** wa mwaka **1996** uliamua Shirika lifanye kazi katika Wilaya yote ya Kiteto badala ya vile vijiji sita vilivyoanzisha shirika.

Mwaka **2005 – 2007** Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika liliamua kupanua shughuli zake kwa mikoa yote ya Tanzania Bara. **KINNAPA** inashirikiana na vikundi vidogo vidogo, serikali za vijiji, Halmashauri za Wilaya,Idara mbali mbali za serikali pamoja mitandao ya mashirika mengine nchini na ulimwenguni.

Shirika la **KINNAPA** lilipokea ruzuku ya kwanza mwaka **1994** kutoka katika Shirika la **NOVIB** la nchini Uholanzi. Kutoka hapa Shirika limekuwa likipata ruzuku na ufadhili kutoka katika mashirika mbalimbali kama vile, **WaterAid, TROCAIRE, TRIAS, MS -Tanzania (sasa hivi ActionAid Tanzania), CARE International, The Foundation for Civil Society, Bernard van Leer Foundation, Banyan Tree Foundation, NAFAKA (USAID), AFRICARE, MISEREOR, WaterCan, UNDP, Water to Thrive, International Indigenous Women's Forum(IIWF), ILRI, IFAD, WFP, EU, MALALA FUND** na Serkali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Kwa kipindi cha miaka 30 shirika limekuwa likitekeleza miradi mbalimbali hasa katika nyanja za Jinsia na Watoto hasa maendeleo ya watoto kwenye umri mdogo (early stimulation for children from 0-8 years of age), Uwezeshaji wa kinamama kiuchumi (Women Socio-economic Empowerment), Usalama wa chakula kwa wawindaji waokota matunda, Maji na Usafi wa mazingira, Usimamizi wa Maliasili na Mazingira, Elimu, Afya, Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Uendelezaji wa mifugo na kilimo, lishe pamoja na shughuli nyingine.

## Dhima ya Shirika:

"Kuchangia katika uboreshaji wa maisha ya wafugaji wa asili, wakulima wadogo wadogo na wawindaji waokota matunda wa Tanzania bara huku likihakikisha kuwa kuna ushiriki wa jamii katika miradi ya maendeleo, usawa wa kijinsia, matakwa ya sera na sheria za Tanzania pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali".

## Viapaumbele vya Shirika :

KINNAPA imejikita katika kufanya shughuli zake katika vipaumbele sita ambavyo ni Maji na Usafi wa Mazingira, Huduma za Kiafya, Maendeleo ya Mifugo na Kilimo, Usimamizi wa Ardhi, Elimu pamoja na uendelezaji wa Shirika.

## Miradi tunayotekeleza kwa sasa :

1:- **WASH IMPROVEMENT PROGRAM** : unaofadhiliwa na **WATER TO THRIVE.**

2:- Participatory Ecosystem Management Project : unaofadhiliwa na **UNDP.**

3:- **Gender Based Violence Prevention and Response** : unaofadhiliwa na **FCS.**

4:- **Amani na Furaha Yangu** : unaofadhiliwa na **Women Fund Tanzania – Trust (WFT).**

5:- **Livestock, Climate and Systems Resilience** : unafadhiliwa na **ILRI/IFAD/EU.**

6:- **Education Champions Network 'NIPE NAFASI'** unaofadhiliwa na **MALALA FUND.**

# <u>MAFANIKO YA SHIRIKA LA KINNAPA.</u>

Shirika la KINNAPA limewafikia zaidi watu **200,000** katika utekelezaji wa shughuli zake ambapo tumewahi kuwa na miradi katika vijiji vyote 63 vya Wilaya ya Kiteto, vijiji na mitaa 87 katika Wilaya ya Simanjiro pia tumetekeleza miradi katika wilaya za Serengeti na Bunda Mkoani Mara, Kilindi na Handeni Mkoani Tanga, Mvomero Mkoani Morogoro, Chemba na Kondoa Mkoani Dodoma, Bagamoyo (Chalinze) mkoani pwani. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na matokeo yake ni:-

**1**:- Kwa kushirikiana na jamii tumeanzisha vituo 42 vya kuendeleza watoto wadogo **(Early Childhood Development (ECD) centers)** ambapo zaidi ya watoto **2,880** wamenufaika.

**2:**- Tumechimba visima virefu 11, mabwawa 4 pamoja na visima vifupi 55 kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya mifugo pamoja na matumizi ya nyumbani.

**3:**- Tumefanikiwa kuwabadilisha tabia na mifumo ya chakula kwa jamii za ***Akie*** hasa kwa kuwafundisha na kuwawezesha kulima na utunzaji wa chakula.

**4**:- Kuanzisha na kuwezesha kiuchumi vikundi 149 ambavyo vimejengewa uwezo wa kujiendesha na kifedha.

**5**:- Tumesaidia shule za msingi 11 na zahanati 2 kupata matenki makubwa ya kuvunia maji kwa ajili ya matumizi ya shule na zahanati.

**6**:- Tumeanzisha na kuwezesha vituo 25 kwa ajili ya kutoa elimu kwa watu wazima hasa katika jamii za kifugaji na wawindaji waokota matunda na hii imesaidia kuzibadilisha jamii katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa hasa kwa kuongeza uelewa wa masuala mbali mbali kwa washiriki.

**7**:- Shirika limetoa msaada wa kusomesha zaidi ya wanafunzi 1,000 kwa kusaidia kupata elimu ya shule ya sekondari mpaka elimu ya juu kutoka kaya maskini pamoja na watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Na hii ni kulipia ada, mahitaji ya shule, nauli na fedha za kujikimu.

**8**:- Kutoa elimu juu ya haki za ardhi, usimamizi bora wa ardhi, mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na usimamizi wa rasilimali.

**9**:- Uanzishwaji wa vitalu vya miti pamoja usambazaji wa miche **300,000** kwa ajili ya kuoteshwa kwenye maeneo ya umma kama vile mashuleni, maeneo ya huduma za afya, magereza, polisi pamoja na maeneo ya watu binafsi.

**10**:- Kuwezesha uanzishwaji wa majukwaa ya vijana na kina mama kwenye kata 20 kwa ajili ya kutetea na kufuatilia ubora wa huduma za afya na elimu.

**11**:- Kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi, Halmashauri na wadau wengine kupitia miradi ya **SRMP** na **PRM** tuliwezeha upatikanaji wa nyanda za malisho zenye ukubwa wa zaidi ya hekta **160,000.**

**12**:- Tumesaidia kupunguza ukatili wa kijinsia katika Wilaya za Simanjiro na Kiteto.

**13**:- Tumewawezesha watoa huduma za afya zaidi ya 300 kuwa na miradi endelevu ili waweze kupata muda wa kuihudumia jamii.

**14**:- Tumewapatia wakina mama wajawazito na wanaonyonyesha zaidi ya **11,000** elimu ya uzazi pamoja na kuwawezesha ili kuboresha lishe na kupunguza utapiamlo.

## UWEZO WA SHIRIKA.

**Kihistoria :**, KINNAPA ni Shirika lililojengwa kwenye misingi imara likiwa na wanachama ***5,800.***

**Kiutendaji :**, KINNAPA ina uzoefu mkubwa katika kupanga na kusimamia miradi, pia lina uzoefu katika uchambuzi wa sera, ushawishi pamoja na ushirikishaji wa jamii katika utekelezaji wa miradi.

**Kiutawala :**, Shirika lina mfumo mzuri na unaojulikana wa maamuzi kama vile Mkutano Mkuu, Vikao vya Bodi, Vikao vya timu ya Menejimenti, Kamati za miradi za KINNAPA pia Shirika lina kanuni za usimamizi.

**Kiufundi :**, Shirika lina ofisi zake moja ikiwa na jengo lake la makao makuu lililopo Wilayani **Kiteto** pamoja na ofisi za kupanga jijini Arusha kwenye jengo la **TNRF**, Pia shirika linamiliki magari 6, pikipiki 3, Mashamba 6 pamoja na watumishi wenye fani mbali mbali.

**Kifedha :**, Shirika lina uwezo wa kusimamia na kutekeleza miradi yenye thamani kati ya shilingi million 600 mpaka bilioni 1 kwa mwaka.